



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



12/05/2022

KUMB. NA. LDC/U.10/1 VOL.II/112

WAKUU WA IDARA NA VITENGO  
S. L. P. 19  
LUDEWA

**YAH: KUFANYIKA KWA MAZOEZI NA MICHEZO KILA WIKI YA PILI YA MWEZI KWA WANANCHI NA MCHAKAMCHAKA, MAZOEZI YA VIUNGO NA VIPINDI VYA MICHEZO**

Tafadhali husika na kichwa cha habari cha hapo juu.

2 Napenda kuwakumbusha kuwa ratiba ya mazoezi na michezo katika Halmashauri yetu ya Ludewa tunaendelea kutekeleza agizo la Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linalohusu uhibitaji wa magonjwa yasiyo ambukiza kupitia mazoezi ya viungo na michezo katika ngazi mbalimbali za taasisi za serikali na binafsi.

3 Aidha, kufuatia maagizo hayo kuhusu mamlaka za Serikali za Mitaa nawakumbusha kuwa mchakamchaka, mazoezi ya viungo na vipindi vya michezo katika shule zote za serikali na binafsi za msingi na serikali kila asubuhi kabla ya kuingia madarasani ili kujenga nidhamu, umoja, uzalendo na ukakamavu kwa kila mwanafunzi. Shughuli zote za mazoezi na michezo zisithiri vipindi vya masomo.

4. **Kwa barua hii napenda kuwajulisha kuwa kutakuwa na mazoezi Jumamosi tarehe 14.05.2022 sehemu ya kukutana itakuwa Bomani saa 11.30 asubuhi.**

Gilbert Ngailo

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

**LUDEWA**  
**Mkurugenzi Mtendaji**  
**Halmashauri ya Wilaya**

**LUDEWA**